

# **HALMASHAURI YA WILAYA YA NACHINGWEA**

## **SHULE YA SEKONDARI YA KUTWA CHIOLA**

S.L.P 105

**NACHINGWEA**

18.12.2020

MZAZI/MLEZI WA .....

SHULE YA MSINGI.....

### **YAH: TAARIFA YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHIOLA KIDATO CHA KWANZA 2021**

Ndugu,

Husika na somo la hapo juu.

Ninafurahi kukutaarifu kwamba mwanao ni mionganini mwa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari katika shule hii Kidato cha Kwanza mwaka 2021. Aidha nampongeza kwa kupata nafasi hii ambapo atawea kutimiza ndoto zake katika maisha.

Katika barua nimeambatanisha na orodha ya mahitaji muhimu ya shule ambayo unapaswa kumtekelezea mwanao ili aweze kusoma vizuri na hatimaye afikie malengo yake. Mzazi/mlezi unashauriwa kusoma kwa makini mahitaji hayo.

Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021** siku ya Jumatatu saa 1:30 asubuhi, hivyo mzazi/mlezi unatakiwa kuripoti na mwanao siku hiyo bila kukosa ili aweze kusajiliwa na kuanza masomo mara moja bila kuchelewa.

Ahsante

.....  
**MWANSELE, D.G**

**MKUU WA SHULE**

**NAKALA:**

- Mkurugenzi Mtendaji (W)

S.L.P 291

**Nachingwea**

- Afisa Mtendaji Kata Chiola

S.L.P 291

**Nachingwea**

## **MAHITAJI YA SHULE**

### **a) Sare za Shule Wasichana**

- (i) Sketi mbili (2) ndefu iwe inakaribia kugusa viatu rangi damu ya mzee mshono wa linda box.
- (ii) Shati mbili nyeupe za mikono mifupi. Kwa wanafunzi Waislamu nusu kanzu ya mikono mirefu ivaliwe na hijabu nyeupe.
- (iii) Viatu vyeusi nya ngozi jozi mbili (2) nya kufunika miguu (sio bajaji)
- (iv) Soksi nyeupe jozi mbili (2).

### **b) Sare za Shule Wavulana.**

- (I) Suruali mbili (2) ndefu zisizo za kupana (modal) rangi ya damu ya mzee.
- (II) Shati mbili nyeupe mikono mifupi.
- (III) Viatu vyeusi nya ngozi nya kufunika miguu jozi mbili.
- (IV) Soksi nyeupe jozi mbili.

### **c) Vifaa nya Taaluma**

- (i) Daftari kubwa ( Counter Books) 'quire' 2 au 3 ziwe kumi (10).
- (ii) Mkebe wa vifaa nya Hisabati (Mathematical set).
- (iii) Ruler na pen za bluu au nyeusi za kutosha.
- (iv) Bunda (rim) moja la karatasi nyeupe kwa ajili ya majaribio na mazoezi kwa vitendo.
- (v) Jalada (file) moja la plastic kwa ajili ya kutunzia mitihani.
- (vi) Kamusi (Dictionary) ya Kingereza kwa Kiswahili.

### **d) Chakula cha Mchana**

- (i) Unatakiwa kuchangia mahindi kilo 40 kwa mwaka.
- (ii) MBAazi au kunde kilo 20 kwa mwaka.
- (iii) Mafuta ya kula lita 2, Vitunguu jagi 2 na Chumvi kilo 2.
- (iv) Fedha taslimu Shs.10,000/= (elfu kumi tu) kwa ajili ya kuwalipa wapishi.

Unatakiwa kuvikabidhi vitu vyote hivi kwa Mjumbe wa Kamati ya chakula ya Wazazi aliye kwenye Kijiji chako. Na kama humfahamu wasiliana na mzazi ye yote mwenye mtoto anayesoma katika shule hii.

### **e) Vifaa nya Usafi wa Mazingira.**

- (I) Fagio moja ya chelewa
- (II) Jembe la mpini imara moja
- (III) Fyekeo moja ,ndoo ya lita 10 (kisado)